

RIPOTI YA PENGO LA UZALISHAJI WA HEWA CHAFU MWAKA WA 2023, UJUMBE MUHIMU

Kadiri athari mbaya kwa hali ya hewa zinavyozidi kuongezeka, [Ripoti ya Pengo la Uzalishaji wa Gesi Chafu Mwaka wa 2023: Rekodi iliyovunjwa – Ongezeko la joto lilizidi zaidi, ila dunia imeshindwa kupunguza uzalishaji wa hewa chafu \(tena\)](#) inaonyesha kuwa ulimwengu unaelekea kushuhudia ongezeko la joto la nyuzijoto kati 2.5 na 2.9 kuliko viwango vya kabla ya viwanda iwapo nchi hazitaimarisha juhudi kufanya zaidi kuliko zilivyoahidi chini ya Mkataba wa Paris. Makadirio ya uzalishaji wa hewa chafu kufikia mwaka wa 2030 ni sharti upunguzwe na angalau asilimia kati 28 na 4 ikilinganishwa na sera zilizopo ili kuweza kufikia malengo ya Mkataba wa Paris ya nyuzijoto 2 na 1.5mtawaliwa. Kudumisha uwezekano wa kufikia malengo ya Mkataba wa Paris kunategemea kuimarisha ukabilianaji wa hali katika muongo huu ili kupunguza pengo la uzalishaji wa hewa chafu. Hii itawezesha malengo kabambe zaidi kufikia mwaka wa 2035 katika awamu inayofuata ya ahadi za kushughulikia mazingira na kuimarisha uwezekano wa kutimiza ahadi za kutozalisha hewa chafu, hali itakayoshughulikia angalau asilimia 80 ya uzalishaji wa hewa chafu duniani.

Ulimwengu unaweka rekodi za joto za kutisha, ambazo zinazidisha matukio mabaya ya hali ya hewa na athari zingine kwa mazingira kote ulimwenguni.

- Mwaka huu, hadi mwanzoni mwa Oktoba, siku 86 zilishuhudia joto la zaidi ya nyuzijoto 1.5 kuliko viwango vya kabla ya viwanda. Septemba ndio mwezi ulioshuhudia kiwango cha juu zaidi cha joto kuwahi kurekodiwa, huku wastani ya joto duniani ikiwa nyuzijoto 1.8 kuliko viwango vya kabla ya viwanda.
- Uzalishaji wa gesi ya ukaa (GHG) uliongezeka kwa asilimia 1.2 kutoka mwaka wa 2021 hadi mwaka wa 2022 na kufikia viwango vipya sawa na Gigatani 57.4 za Kaboni Dioksidi (GtCO_{2e}).
- Vivyo hivyo, Uzalishaji wa GHG katika nchi zote za G20 uliongezeka kwa asilimia 1.2 katika mwaka wa 2022.
- Uzalishaji wa hewa chafu unasalia kusambaa kwa njia isiyo na usawa ndani na kati ya nchi, na kuashiria ruwaza ya kimataifa ya ukosefu wa usawa.

Licha ya ongezeko la majanga ya mazingira, juhudi zisizotosha za kukabiliana na hali hii inamaanisha dunia inaenda kushuhudia ongezeko la joto zaidi ya malengo ya kimataifa ya mazingira katika karne hii.

- Iwapo jitihada za kukabiliana na hali kwa kuzingatia sera zilizopo zitaendelea zilivyo, ongezeko la joto duniani litadhibitiwa tu hadi nyuzijoto 3 kuliko viwango vya kabla ya viwanda katika karne hii.
- Utekelezaji kikamilifu na juhudi zinazoendelea kwa kuzingatia Ahadi Zinazowekwa na Taifa (NDCs) zitawezesha ulimwengu kudhibiti ongezeko la joto hadi nyuzijoto 2.9.
- Mafanikio zaidi na uendelezaji wa NDC zilizo na masharti vinaweza kusababisha joto kutozidi nyuzijoto 2.5 kuliko viwango vya kabla ya viwanda.
- Hata tukiwa na matumaini zaidi, ikiwa NDC zote zilizo na masharti na ahadi za kutozalisha hewa chafu zikitimizwa, kudhibiti ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 2.0 kunawezekana. Hata hivyo, ahadi za kutozalisha hewa chafu hazizingatiwi kwa sasa: hakuna nchi yoyote kati ya nchi za G20 inapunguza uzalishaji wa hewa chafu kwa kasi inayorandana na malengo yao ya kutozalisha hewa chafu.

- Hata tukiwa na matumaini zaidi, uwezekano wa kudhibiti ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 1.5 ni asilimia 14.

Dunia inahitaji kupunguza uzalishaji wa hewa chafu kufikia mwaka wa 2030 kwa asilimia 28 ili kupunguza gharama za kuweza kufikia lengo la Mkataba wa Paris la nyuzijoto 2 na asilimia 42 kufikia lengo la nyuzijoto 1.5.

- NDC zinazotolewa kwa hiari na zile zinazotolewa kwa masharti zinakadiriwa kupunguza uzalishaji wa hewa chafu duniani kufikia mwaka wa 2030 kwa asilimia 2 na 9 mtawalia, ikilinganishwa na sera zilizopo tukichukulia kuwa kutakuwa na utekelezaji kikamilifu.
- NDCs zilizopo sisizo na masharti zinaonyesha kuwa upunguzaji wa ziada wa uzalishaji wa GtCO₂e 14 unahitajika kufikia mwaka wa 2030 kuliko viwango vilivyotabiriwa ili kufikia nyuzijoto 2. Upunguzaji wa GtCO₂e 22 unahitajika ili kuweza kufikia nyuzijoto 1.5.
- Utekelezaji wa NDC zilizo na masharti hupunguza makadirio haya yote kwa GtCO₂e 3.

Kuna hatua zimepigwa tangu kutiwa saini kwa Mkataba wa Paris, ila kuimarisha utekelezaji kwa kiwango kikubwa katika muongo huu ni njia ya pekee ya kudhibiti ongezeko la joto duniani lisizidi nyuzijoto 1.5 bila kuongezeka kwa kiwango zaidi.

- Hatua za kisera zimepunguza pengo la utekelezaji, linalofafanuliwa kama tofauti kati ya makadirio ya uzalishaji wa hewa chafu chini ya sera zilizopo na utekelezaji wa NDC kikamilifu.
- Uzalishaji wa GHG katika mwaka wa 2030 kwa kuzingatia sera zilizopo ulitarajiwa kuongezeka kwa asilimia 16 wakati wa kupitishwa kwa Mkataba wa Paris. Sasa makadirio ya ongezeko ni asilimia 3.
- Pengo la utekelezaji duniani kufikia mwaka wa 2030 linakadiriwa kuwa GtCO₂e 1.5 kwa NDC za hiari (likipungua kutoka GtCO₂e 3 mwaka jana), na GtCO₂e 5 zitawezesha kwa NDC zilizo na masharti (likipungua kutoka GtCO₂e 6).
- Nchi tisa zimewasilisha NDC mpya au zilizosasisiwa tangu COP27 mwaka wa 2022, na hivyo kufanya jumla ya idadi ya NDC zilizosasisiwa kuwa 149.
- Ikiwa NDC zote mpya na zilizosasisiwa zisizo na masharti zitatekelezwa kikamilifu, inakadiriwa zinaweza kupunguza uzalishaji wa GHG kwa takriban GtCO₂e 5.0 kila mwaka kufikia mwaka wa 2030, ikilinganishwa na NDC za awali. NDC tisa zilizotolewa tangu COP27 hukadiriwa takribani GtCO₂e 0.1 ya kiasi hiki.
- Hata hivyo, bila viwango vya uzalishaji wa hewa chafu kupunguzwa zaidi kufikia mwaka wa 2030 ikilinganishwa na viwango vinavyokadiriwa na utekelezaji wa NDC kikamilifu, haitawezekana kupata njia za gharama nafuu za kudhibiti ongezeko la joto duniani lisizidi nyuzijoto 1.5 kuliko viwango vya kabla ya viwanda, na fursa ya angalau asilimia 33, katika karne hii.

Mataifa yote yanapaswa kuimarisha maendeleo ya mabadiliko ya kupunguza hewa ya ukaa katika uchumi wote

- Nchi zilizo na uwezo mkubwa na huchangia zaidi kwa uzalishaji wa hewa chafu – hasa nchi za kipato cha juu na nchi zinazozalisha hewa chafu nyingi kati ya nchi za G20 – zitahitaji kuchukua hatua kabambe kwa dharura na kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa mataifa yanayoendelea.
- Kwa vile nchi za kipato cha chini na cha kati tayari zinachangia zaidi ya theluthi mbili ya uzalishaji wa GHG duniani, na kukidhi mahitaji ya maendeleo yalio na uzalishaji mdogo wa hewa chafu.
- Makaa ya mawe, mafuta na gesi inayochimbwa katika kipindi chote cha uzalishaji na mipango ya kuchimba migodi na maeneo ya uchimbaji vinaweza kuzalisha zaidi ya mara 3.5 ya bajeti iliopo

ya hewa ya ukaa ya kudhibiti ongezeko la joto lisizidi nyuzijoto 1.5, na karibu bajeti yote iliopo ya kufikia nyuzijoto 2.

Nchi za kipato cha chini na cha kati hukabiliwa na changamoto za kiuchumi na kitaasisi wakati wa mabadiliko ya nishati inayozalisha kiwango cha chini cha hewa ya ukaa lakini pia zinaweza kutumia fursa.

- Mabadiliko katika nchi za kipato cha chini na cha kati yanaweza kusaidia kuwezesha ufikiaji wa nishati kwa wote, kuondoa mamilioni ya watu kutoka lindi la umaskini na kupanua viwanda vilivyo na mikakati.
- Maendeleo yanayohusishwa na nishati yanaweza kutekelezwa kikamilifu na kwa usawa huku nishati inayozalisha kiwango kidogo cha hewa ya ukaa kama nishati jadidifu ikiwa nafuu, na kuhakikisha kuna ajira isiyochafua mazingira na hewa safi.
- Msaada wa ufadhili wa kimataifa utalazimika kuongezwa kwa kiwango kikubwa, huku vyanzo vipya vya mtaji vya umma na vya kibinafsi vikifanyiwa marekebisho kupitia mifumo ya ufadhili ya kupunguza gharama za mtaji. Inajumuisha ufadhili wa madeni, ufadhili ulio na masharti nafuu wa muda mrefu, dhamana na fedha za kuimarisha hali.
- Maandalizi ya awamu inayofuata ya NDCs yanatoa fursa kwa nchi za kipato cha chini na cha kati kuweka mikakati ya kitaifa kwa kuzingatia hali katika nchi zao ya sera kabambe na hatua za kushughulikia mazingira, na shabaha ambazo mahitaji ya fedha na teknolojia vinabainishwa wazi.
- COP28 inapaswa kuhakikisha kwamba msaada wa kimataifa unatolewa ili kukuza mikakati ya aina hii.

Tathmini ya kwanza ya Kimataifa (GST) katika COP28 itatoa mfumo wa kukuza ahadi.

- Tathmini ya kwanza ya Kimataifa (GST) chini ya Mkataba wa Paris itakuwa nguzo kwa awamu inayofuata ya NDC ambazo nchi zinapaswa kuwasilisha katika mwaka wa 2025 na malengo ya mwaka wa 2035.
- Kuchukua hatua katika muongo huu kutaamua kujitolea kunakohitajika katika NDC hizi, na uwezekano wa kufikia malengo ya muda mrefu ya joto katika Mkataba wa Paris.
- Ahadi za kimataifa katika awamu inayofuata ya NDC ni sharti zifanye uzalishaji wa GHG kufikia mwaka wa 2035 kurandana na viwango vya chini ya nyuzijoto 2 na nyuzijoto 1.5, huku zikifidia uzalishaji wa ziada hadi viwango vinavyowiana na hali hii kufikiwa.

Kuchelewesha upunguzaji wa uzalishaji wa GHG kutaongeza utegemezi wa siku zijazo kwa kuondolewa kwa kaboni dioksidi kutoka angani.

- Njia zote zinazorandana na utumizaji wa malengo ya Mkataba wa Paris zinahitaji upunguzaji mkuu wa dharura wa uzalishaji wa hewa ya ukaa na matumizi ya chombo cha kuondoa kaboni dioksidi (CDR) kwa kipindi kirefu.
- Uondoaji wa kaboni dioksidi tayari unatekelezwa, hasa kupitia upandaji miti, kurejesha misitu na usimamizi wa misitu. Uondoaji wa sasa wa moja kwa moja kupitia mbinu za juu ya ardhi unakadiriwa kuwa GtCO₂e 2.0 kila mwaka.
- Mbinu za gharama nafuu zitapelekea uongezaji wa njia za kawaida na njia mpya za CDR, ila kufikia viwango vya juu vya uondoaji wa CDR bado haziko dhahiri na huhusishwa na madhara: kuhusu ushindani wa ardhi, ulinzi wa umiliki na haki ya kumiliki na mambo mengine.

- Kuimarisha mbinu mpya za uondoaji wa kaboni dioksidi huhusishwa na aina mbalimbali ya madhara, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya kiufundi, kiuchumi na kisiasa ili kutekeleza kwa kiasi kikubwa huenda visitokee kwa wakati.
- Hii inaashiria maeneo manne muhimu yanayohitaji hatua za kisiasa: kuweka na kuashiria vipaumbele vya CDR; kuendeleza mifumo thabiti ya ufuatiliaji, kuripoti na uthibitishaji ili kuongeza uaminifu; kutumia ushirikiano na faida pamoja na juhudi zingine; na kuongeza kasi ya uvumbuzi.